

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S.L.P 42325,
Simu Nambari: 2850633
Nukushi: (022) 2850635
Barua Pepe: rbctemeke@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

02/06/2020

MWENYEKITI WA KAMATI YA MAZINGIRA MTAU WA TAMBUKARELI
MBARONI KWA KOSA LA KUOMBA NA KUPOKEA RUSHWA

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Temeke jijini Dar es Salaam imemkamata Mwenyekiti wa kamati ya Mazingira wa Mtaa wa Tambukareli Kata ya Azimio kwa kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu kinyume na kifungu cha 302 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marebicho mwaka 2002.

Mnamo tarehe 19/01/2019 ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Temeke ilipokea malalamiko yanayomhusu ALLY MOHAMED MTIGA ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira Mtaa wa Tambukareli Kata ya Azimio anayejifanya ni Afisa wa Ardhi kuwa anaomba rushwa Shilingi 200,000/= kutoka kwa Mwananchi (jina limehifadhiwa) ili aweze kumsaidia kupata leseni ya makazi ya jengo lake.

Uchunguzi wa TAKUKURU ulibaini kwamba, mnamo tarehe 26/01/2019 Ally Mohamed Mtiga ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mazingira Mtaa wa Tambukareli Kata ya Azimio anayejifanya Afisa wa Ardhi, akiwa ofisini kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Tambukareli alipokea fedha hizo za mtego kiasi cha Shilingi 200,000/= ili aweze kumsaidia mwananchi mmoja (jina limehifadhiwa) kupata leseni ya makazi ya jengo lake.

Uchunguzi wa tuhuma hii umekamilika na mtuhumiwa anatarajiwa kufikishwa mahakamani siku ya Jumatano tarehe 03/06/2020 na kufunguliwa mashitaka kwa kosa la kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu kinyume na kifungu cha 302 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura namba 16 kama ilivyofanyiwa marekebicho mwaka 2002, katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke.

TAKUKURU Mkoa wa Temeke inatoa wito kwa wananchi wote kuendelea kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia mitandao yote ya simu kwa kupiga au kutuma ujumbe mfupi kwa namba ya bure 113 au kupiga 113 au kufuata maelekezo au fika katika ofisi ya TAKUKURU iliyopo karibu nawe.

KATAA RUSHWA, JENGA NCHI YAKO

Imetolewa na:

Donasian Kessy

Mkuu wa TAKUKURU (M)

Temeke